**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KANTALAMBA – SUMBAWANGA,RUKWA.

**JANUARY, 2026.**

**KANTALAMBA SS.- SUMBAWANGA,RUKWA.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule 0754357996**

**Makamu Mkuu wa Shule 0762852383**

**Patron 0767501755**

**Shule ya Sekondari KANTALAMBA**

**S.L.P. 70**

**Tarehe 21/11/2025**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………………………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KANTALAMBA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA, MKOA WA RUKWA, MWAKA 2026**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2026. Ninachukua nafasi hii kukupongeza kwa jitihada zako zilizowezesha kustahili uchaguzi huu. Nitegemeo langu kwamba jitihada hizo zitaendelea awapo katika shule hii.

**2.** Shule ya Sekodari Kantalamba ipo katika Manispaa ya Sumbawanga. Manispaa hii ambayo ni makao Makuu ya mkoa wa Rukwa ipo umbali wa kilometa 336 toka Mbeya na kilometa 240 toka Mpanda. Upo usafiri wa uhakika kila siku toka Mbeya ambapo mabasi huondoka kuanzia saa 12:30 alfajiri na kuwasili Sumbawanga saa 7:00 mchana.

Kutoka Mpanda usafiri upo kila siku ambapo gari huondoka saa 1:00 asubuhi na kuwasili Sumbawanga saa 7:00 mchana,**LAKINI PIA UPO USAFIRI WA UHAKIKA KUTOKA DODOMA AU DAR ES SALAAM HADI MJINI SUMBAWANGA**. Shule ipo umbali wa kilometa tatu (3) kutoka katikati ya mji. Kwa kutumia usafiri wa tax utalipa shs.5,000/= na kwa kutumia bajaji utalipa shs. 700/=.
Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **13/01/2026**. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **12/01/2026.**

## 3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 3.1 SARE ZA SHULE

i. **SURUALI 1 DARK BLUE**: Yenye malinda mawili kila upande na mkunjo au pindo chini (turn up) na isiyobana.

ii. **SURUALI 1 KAKI:** Yenye malinda mawili kila upande na mkunjo au pindo chini (turn up) na isiyobana.

iii. **SURUALI 1 NYEUSI (YAKUSHINDIA):** Yenye malinda mawili kila upande na mkunjo au pindo chini (turn up) na isiyobana..

iv. **TAI 2**: Rangi dark blue na kaki

**v. SHATI 2 ZA RANGI NYEUPE:**
Mikono mirefu lenye mfuko mmoja kifuani upande wa kushoto.

**vi. VIATU:**
❖ Rangi nyeusi vyenye kamba, visiwe na soli nene, hairuhusiwi kuvaa viatu vya matairi,
❖ Kandambili au yeboyebo wakati wa masomo darasani na bwaloni/ukumbi wa chakula, haviruhusiwi.

**vii. SOKSI:**
❖ Rangi nyeusi isiyo na urembo wowote.

**viii. MKANDA:**
❖ Rangi nyeusi na uwe wa ngozi
❖ Usiwe na madoa au urembo wowote.

**ix. T.SHIRTS:**
❖ Rangi ya blue yenye kola

x. **SWETA:** Rangi ya blue
**NEMBO NA CHATA ZINAPATIKANA SHULENI KWA GHARAMA NAFUU**

xi. **NGUO ZA MICHEZO**

Anatakiwa aje na nguo za michezo ambazo ni:-

- Bukta na fulana zote rangi ya bluu,
- Track suit rangi nyeusi.
- Raba kwa ajili ya michezo

**NB: Hairuhusiwi kuja na nguo za nyumbanI**

## 3.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI

**MAHITAJI YA BWENINI.**

i. Ggodoro futi 2½
ii. Chandarua.
iii. Mashuka mawili au zaidi ya rangi ya blue bahari.
iv. Taulo, blanketi na Sanduku la chuma (original).

**MAHITAJI YA NYARAKA ZA SERIKALI.**

i.Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
ii.Aje na FORM YA UTAMBULISHO KATIKA KATIKA OFISI ZA SERIKALI ZA MITAA IKITAMBULISHA WAZAZI/WALEZI WAKO..

**MAHITAJI YA VIFAA VYA USAFI**.

i. Ndoo mbili za lita 10 kwa ajili ya kuchotea maji ya chooni na usafi binafsi.
ii. Drier/Mopa au brashi ya chooni
iii. Jembe moja lenye mpini

**MAHITAJI YA KITAALUMA**

i.Madaftari aina ya counter book kumi na mbili kwa ajili ya nukuu za masomo.
ii.Kalamu za kutosha.Ziwe nyeusi au blue.
iii.**Rimu 2** za karatasi kwa ajili ya kufanya mitihani na mazoezi mbalimbali.Unaweza kuja na moja kwa muhula mmoja na nyingine utakuja nayo muhula wa pili.

**BIMA YA AFYA**.

Mzazi hakikisha umemkatia **BIMA YA AFYA** mwanao na aje nayo siku ya kuripoti.Na kama ukishindwa,hapa shuleni kuna utaratibu wa kuwasajili wanafunzi kwenye bima ya afya kwa kuwaita maafisa wa bima ya afya na kuja kuwasajili wanafunzi hapa hapa shuleni kwa pamoja.Gharama yake ni tshs 53,000/.Kwa hiyo unapomleta mtoto hakikisha amekuja na kadi ya **BIMA YA AFYA** au kiwango hicho kilichotajwa hapo juu.

## 4. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. **Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni**.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**

❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**5. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**6.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………….**

**Jina la Mkuu wa Shule ……………………………………..**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0754357996**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0762852383**
- **Mwandamizi Taaluma 0755076645**
- **Mwandamizi Malezi 0755262311.**

**PRESIDENT"S OFFICE- REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.**

KANTALAMBA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 70,
**SUMBAWANGA**
DATE……………………………………

MEDICAL OFFICER
GOVERNMENT HOSPITAL
……………………………………
……………………………………

**REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Name ……………………………………………………………………………………………

Please examine the above named as to HIS/HER physical and mental fitness as indicated below and arrange for necessary treatment if required. This certificate must be signed by qualified medical officer of a government Hospital and returned to school by the student.
The examination should include the following categories:

1. Sight
2. Hearing
3. Hemoglobin
4. Blood pressure
5. Pulmonary tuberculosis
6. Neurosis
7. Venereal diseases
8. Skin diseases
9. Urine
10. Leprosy
11. Any disability
12. Stool
13. Pregnancies test
14. Other serious disease

MEDICAL CERTIFICATE
( To be completed by a Government Medical Officer)

- I have examined the above named student and consider that she /he is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full schooling.
- Other comments………………………………………………………………………………

Date …………………………………

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**OFISI YA RAIS.**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**

**SHULE YA SEKONDARI KANTALAMBA,**
**S. L. P. 70,**
**SUMBAWANGA**.

**FOMU YA MWANAFUZI YA KUKIRI NA KUKUBALIANA NA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE;**
(**Fomu hii ijazwe na mwanafunzi husika**).

**SEHEMU YA KWANZA**.

Jina la mwanafunzi (matatu)………………………………………………………………………

Tarehe ya kuzaliwa;...............................................................................................
Dini;.................................................................................................................
Majina kamili ya mzazi /mlezi unayeishi naye;.........................................................
Anuani ya nyumbani;..............................................wilaya.....................................
mkoa…………………...............
Shule anayotoka;............................................................................................
Na. ya/za simu za wazazi/walezi;.......................................................................
Jina la mwenyekiti wa mtaa anakotoka;.......................................................................
Na ya simu ya mwenyekiti wa mtaa anakotoka mwanafunzi;..................................
Jina la mtu mwingine wa karibu;...........................................................................
Mahali anapoishi;.............................................................................................
Uhusiano wenu;..................................................................................................
Namba yake/zake za
simu;..............................................................................................................

**SEHEMU YA PILI.**

**Kiapo cha mwanafunzi.**

Mimi ………………………………………………………………………….. Nakiri kusoma na kuelewa maelekezo na sheria zote za nchi na shule zilizoainishwa hapo juu. Ninaahidi kutii na kufuata sheria zote kama zilivyoainishwa. Endapo nikikiuka sheria izo hatua kali zichukuliwe kwa mujibu wa sheria husika.

**EE MWENYEZI MUNGU NISAIDIE!!!!!**

Saini…………………………………………………
Tarehe…………………………………………………..

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**OFISI YA RAIS.**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**

**SHULE YA SEKONDARI KANTALAMBA,**
**S. L. P. 70,**
**SUMBAWANGA**.

**FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI NA KUKUBALIANA NA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE;**
(**Fomu hii ijazwe na mzazi/mlezi wa mwanafunzi**)

MAJINA MATATU YA MZAZI;..........................................................................

ANUANI
KAMILI…………………………………WILAYA………………………MKOA…………………………..
NAMBA ZA SIMU;……………………………………………………………………….
BARUA PEPE…………………………………………………………………………………………………

**UKIRI WA MZAZI**

Mimi…………………………………………………………………………………mzazi/mlezi wa mwanafunzi………………………………………………………………..kwa akiri zangu timamu nimesoma na kuelewa sheria na taratibu zote za shule. Nakubalina nazo na naahidi kutoa ushirikiano mzuri endapo changamoto yoyote itajitokeza na kukubaliana na adhabu yoyote itakayotolewa kwa mtoto wangu kwa mujibu wa sheria na kanuni za shule zilizowekwa.

**EEE MWENYEZI MUNGU NISAIDIE!!!!!**

JINA KAMILI………………………………………………………………
Saini ………………………………………………………………………..
Tarehe……………………………………………







SURUALI YA KAKI NA TAI

SURUALI YA DARK BLUE NA TAI




**T.SHIRTS RANGI YA BLUE YENYE KOLA**



SWETA RANGI YA BLUE



SURUALI  RANGI NYEUSI